# WILAYA YA MAKUENI

# DARASA LA NNE MUHULA WA TATU

PENPLUS MAKUENI

# KISWAHILI

***Muda: Saa 1 Dakika 40***

***Chagua jibu linalofaa kujaza mapengo yaliyoachwa wazi kutoka nambari 1-15.***

Maisha ya __1__ yalimfurahisha sana Kizito. Aliringa kama __2__ kwa rafiki __3__. Alicheka na kila __4__ aliyemwona. Siku moja, Kizito __5__ darasani aliulizwa aeleze punda ni __6__. Kwanza alicheka __7__ akasema __8__ uchangamfu kuwa "punda ni noti __9__ zikifungwa pamoja, yaani punda la noti". Kila mtu darasani __10__ kicheko kama radi.


1. A. shule B. shuleni C. kwa shule D. kwenye shule
2. A. teusi B. kasuku C. tausi D. tauni
3. A. wake B. wao C. wetu D. zake
4. A. moja B. watu C. mmoja D. kitu
5. A. akiwa B. akikuwa C. akikua D. awe
6. A. nani B. nini C. gani D. wapi
7. A. kisha B. kisa C. kicha D. alafu
8. A. na B. wa C. ni D. kwa
9. A. mingi B. mengi C. nyingi D. vingi
10. A. aliagua B. aliangua C. aliungua D. aliugua

Mtoto __11__ aliacha mchezo __12__ aliokuwa __13__ na akafuata maneno __14__ __15__.

11. A. ule B. yule C. wale D. vile
12. A. yake B. zake C. wake D. lake
13. A. anayo B. nalo C. nako D. nao
14. A. aliyokuwa B. aliokuwa C. alizokuwa D. alilokuwa
15. A. akiifuata B. akizifuata C. akiyafuata D. akiufuata

***Kutoka swali la 16-30 chagua jibu sahihi kulingana na maagizo.***

16. Neno maradhi liko katika ngeli gani?
    A. YA - YA B. LI - YA C. KI - VI D. U - YA
17. ***Tegua kitendawili.*** Mama nieleke. ______
    A. Kitanda B. Usingizi C. Gari D. Mimba
18. _____ niazime kalamu yako, yangu imepotea.
    A. Pole B. Tafadhali C. Niwie radhi D. Samahani
19. ***Jaza pengo.***
    Niazime maziwa __________ niyanywe.
    A. chache B. madogo C. kidogo D. mingi
20. Chagua sentensi sahihi.
    A. Mimi ndimi nilimsaidia
    B. Mimi ndiye niliyomsaidia
    C. Mimi ndimi niliyemsaidia
    D. Mimi ndiye nilimsaidia
21. ***Kanusha sentensi hii.***
    Umekula nilichokupikia.
    A. Hujakula ulichonipikia
    B. Hujala ulichonipikia
    C. Hujakula nilichokupikia
    D. Hujala nilichokupikia
22. Ni jina lipi halifai kati ya haya?
    A. Shubaka B. Shajara C. Zulia D. Kochi
23. Ni upi si mmea?
    A. Mbuni B. Shayiri C. Ndizi D. Mchai
24. Nitamwitaje mke wa mtoto wangu?
    A. Shemeji B. Mavyaa C. Kining'ina D. Mkazamwana
25. Thumuni huandikwaje?
    A. $^1/_7$ B. $^1/_5$ C. $^1/_8$ D. $¼$
26. Mbung'o huambukiza maradhi ya ______
    A. kifafa B. ukoma C. safura D. malale
27. Andika wingi wa "**uso mfupi**"
    A. Nyuso fupi B. Mauso fupi C. Nyuso fupi D. Nyuso mfupi
28. Umbo hili ni ____________



    A. duara B. mche C. pia D. hiramu
29. Kipofu yule alikuwa na nywele ________
    A. ndefu B. refu C. ndevu D. mrefu
30. Mimi ni vazi la kike linalovaliwa ndani ya rinda. Basi mimi ni ____________
    A. shimizi B. kitenge C. bombo D. kanchiri

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali ya 31-40.*

Nyuki huishi ndani ya mzinga. Kila nyuki huwa na kazi maalumu ambayo huwa amegaiwa. Kuna wale ambao huenda kwenye maua kutafuta asali, kuna wale ambao huenda kutafuta maji, wengine huwa askari na kadhalika. Mzinga wa nyuki huwa na asali ambayo ni chakula cha nyuki wachanga. Watu wanapojaribu kwenda kuichukua asali kutoka kwenye mzinga, nyuki huwauma.

Asali ya nyuki hutumika kama chakula na binadamu. Ni tamu sana. Watu wanapotaka kuonyesha kuwa kitu ni kitamu, husema ni kitamu kama asali. Siku hizi, nyuki hufugwa. Kuna shule ambazo hujipatia pesa nyingi kwa kuwaweka nyuki katika mashamba ya shule. Wanafunzi wanapokwenda kuchukua asali, huvaa nguo za kujizuia wasiumwe na nyuki. Mtu akiumwa na nyuki wengi anaweza kufariki.

Siku za mababu zetu asali ilitumiwa kutengeneza pombe, kulika kama chakula na hata kutibu magonjwa.

31. Makao ya nyuki ni __________
   A. nje ya mzinga B. ndani ya mzinga
   C. katika maua D. kando ya mzinga
32. Nyuki wote huwa na __________
   A. kazi fulani B. maji mengi
   C. asali nyingi D. maua mengi
33. Ndani ya mzinga hupatikana:-
   A. maua B. asali
   C. maji D. askari pekee
34. Tunaposema kitu ni kitamu kama asali, tuna maana kuwa:-
   A. ni kizuri sana B. ni kitamu sana
   C. si kitamu D. kinapendeza
35. Nyuki hufugwa __________
   A. nyumbani B. katika majumba ya shule
   C. jikoni D. katika mashamba ya shule
36. Wanafunzi wanapokwenda kuchukua asali
   A. Hawavai nguo za kujizuia wasiumwe na nyuki
   B. Huvaa nguo za kujizuia wasiumwe na nyuki
   C. Huvaa nguo zote
   D. Hujipaka mafuta ili wasiumwe na nyuki
37. Mtu akiumwa na nyuki wengi anaweza:-
   A. kufa B. kunona
   C. kupata usingizi D. kucheka sana
38. Asali hutumiwa kwa njia gani?
   A. Kuoga B. Kula C. Kufagia D. Kulala
39. Tamu kama __________
   A. asali B. sukari C. chakula D. muwa
40. Kichwa cha hadithi hii ni:-
   A. Ufugaji wa nyuki B. Asali ya nyuki
   C. Kuumwa na nyuki D. Kula asali

*Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali ya 41-50.*

Kasuku ni ndege wa ajabu sana. Ana uwezo wa kuyarudisha maneno anayosikia yakisemwa na watu kwa mfano, ukisema "Jambo", kasuku atakujibu, "Jambo". Hadija na wenzake walikuwa wakicheza na Kasuku wao, walipousikia mlio wa gari nje ya nyumba yao. Watu wanne walitoka na kuanza kuinyemelea nyumba yao.

"Mwizi! mwizi! Kasuku alisema. Kulisikia onyo hilo. Hadija alikimbia na kuufunga mlango. Baada ya kufunya hivyo, yeye na mwenzake walijifungia ndani ya kabati na kunyamaza kimya kabisa. "Fungua," mmoja wa wezi hao aliamuru. Kasuku ali-mjibu "fungua." Jibu hilo liliwakasirisha wezi hao.

"Mtaufungua mlango au mnataka tuingie kwa nguvu?" Mwizi huyo aliuliza kwa hasira kwa vile kasuku hakuweza kuyambuka yote yaliyosemwa alirudia sehemu ya mwisho kusema, "....mnataka tuingie kwa nguvu?" Mazungumzo haya yalipokuwa yakiendelea, wazazi wa Hadija walifika na kuwakamata wezi hao. Walipoelezwa kuwa kasuku ndiye aliyewasaidia wazazi walifurahi sana. Walimwendea na kumwambia "Asante sana". Naye aliwajibu kwa sauti nyororo na kusema "Asante sana."

41. Kasuku ni ndege wa ajabu kwa sababu:-
   A. huweza kuruka
   B. ana mbio sana
   C. hana uwezo wa kusema
   D. ana uwezo wa kusema
42. Hadija na wenzake walipousikia mlio wa gari, walikuwa:-
   A. wakisikiliza
   B. wanacheza
   C. wakiwangojea wazazi
   D. wakiwangojea wazazi wao
43. Waliokuja na gari walikuwa watu:-
   A. watano B. watatu C. wanane D. wanne
44. Aliyesema "mwizi! mwizi" ni __________
   A. kasuku B. Hadija
   C. wenzake Hadija D. Hadija na wenzake
45. Baada ya kufunga mlango, Hadija na wenzake:-
   A. walitoroka B. walitoka nje
   C. walijificha D. waliingia garini
46. Kasuku alipowajibu wezi na kuwaambia "fungua", wezi hao:-
   A. walifurahi B. walifungua mlango
   C. walicheka D. walikasirika
47. Wezi hao walitisha:-
   A. kuingia kwa nguvu
   B. kwenda zao
   C. kuwapiga Hadija na mwenzake
   D. kumpiga kasuku
48. Mwenzake Hadija aliitwa __________
   A. Rehema B. Amina C. Hatujaambiwa D. John
49. Tunasema siku za mwizi ni __________
   A. Thelathini B. Arubaini C. Saba D. Kumi
50. Kichwa mwafaka cha ufahamu huu ni:-
   A. Uzuri wa Kasuku B. Ubaya wa Kasuku
   C. Wezi nyumbani D. Hadija ma mwenzake